**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(TAMISEMI)**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA**
**SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MUSOMA.**
**S.L.P 54 MUSOMA.**
**SIMU : 0755 671818, 0767 082905.**
**Email:musomatechsecondaryschool@gmail.com**

**YAH: MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MUSOMA MWAKA 2023.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ……………. na atasoma tahasusi ya …………

Shule ya Sekondari **MUSOMA UFUNDI** ipo umbali wa Kilometa 04 Kutoka makao makuu ya Manispaa ya Musoma na Kilomita 07 kutoka Stendi kuu ya Mabasi Bweri Usafiri wa dalala kutoka mjini na kutoka kituo cha mabasi Nauli ni Shilingi 500 kwa pikipiki na Shilingi 2000 kwa bajaji Shilingi 1000.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **14/08/2023** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 14/08/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/08/2023.** Mara mwanafunzi afikapo shuleni **aripoti Ofisini kwa Makamu Mkuu wa Shule kwa mapokezi na usajili.**

Pia mwanafunzi ajapo shuleni ni muhimu aje na vitu vifuatavyo;

i. Kivuli cha Cheti cha Kuzaliwa kinachotolewa na Serikali (copy of Birth Certificate).
ii. Fomu iliyojazwa na Daktari kuhusu Afya ya Mwanafunzi (Medical Examination Form).
iii. Fomu iliyojazwa ya maelezo binafsi ya mwanafunzi (Personal Particularas Form).
iv. Fomu ya kukubali masharti ya shule. Wewe na mwanao muisome kwa kina pamoja na sheria za shule mkizikubali,
msaini fomu hizo na ziwasilishwe shuleni hapa wakati wa kuripoti.
v. Kivuli cha Cheti cha kumaliza Kidato cha Nne (Leaving Certificate).
vi. Kivuli cha matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne
(Result Slip).
vii. **Picha nne (04) “Passport Size” za Mwanafunzi na Picha moja moja “Passport Size” za Wazazi na ndugu wa karibu wa Mwanafunzi wanaoweza**

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### A.SARE ZA SHULE

i. Mashati mawili meupe yenye **mikono Mirefu**.
ii. Suruali mbili nyeusi zenye mifuko miwili ya pembeni na mmoja nyuma kulia zisizobana na zisiwe **"Jeans"** wala **"Modo"** Upana wa chini usipungue **inchi "15" ukipungua hiyo suruali itachanwa.**
iii. **Tshirt mbili (2) za kushindia baada ya masomo rangi ya blue zenye kola nyeusi (Zinapatikana shuleni kwa Tsh 12000).**
iv. **MUHIMU: Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kuwa na nguo za nyumbani shuleni.**
v. Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba jozi 2 visiwe na kisigino kirefu wala shingo ndefu.
vi. Soksi jozi 2 rangi nyeusi.
vii. Sweta ya rangi ya kijani kibichi (Rangi ya mimea) yenye alama ya "V" shingoni. (**Zinapatikana maeneo ya shule kwa Tsh 12,000/=)**
viii. Suruali ya rangi ya damu ya Mzee– huvaliwa baada ya saa za masomo.
ix. Aje na viatu na nguo za michezo. Bukta, Tshirt ya rangi ya Blue na track za rangi ya blue (zinapatikana karibu na shule)
x. Mkanda wa ngozi rangi nyeusi au ugolo wa ukubwa wa kati usio na "bicross" kubwa.
xi. Tai mbili nyeusi **(Zinapatikana maeneo ya shule.)**
xii. **NB. Mwanafunzi wa shule hii hapaswi kuja na nguo nyingine yoyote tofauti na hizo hapo juu. Nguo za nyumbani hazitakiwi kabisa shuleni hapa.**

### B. VIFAA BINAFSI

**VIFAA VYAKE BINAFSI VYA KUTUMIA BWENINI**

1. **Godoro** la **<u>"Sponge" la 2.5ft x6"(unene ni nchi 6) hakikisha unaleta godoro lililoagizwa kwa size hiyo</u> (Zinapatikana maeneo ya shule endapo utashindwa kupata huko uliko zingatia vipimo).**
2. Shuka mbili mpya rangi moja ya bluu bahari (Light blue).
3. Mto na foronya ya rangi ya blue bahari.
4. Chandarua (Vitanda vyetu ni Futi 2.5)
5. Ndala/Kandambili
6. Taulo
7. Sanduku la bati kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake ni (lazima)
8. Ndoo moja ya kuchotea maji na dumu la lita 5 kwa ajili ya kutunzia maji yake ya kunywa (Lazima).
9. Mwanafunzi aje na Toilet paper walau 10 kwa matumizi yake.
10. Sahani, bakuli, Kijiko na Kikombe cha nusu lita .
11. Fedha za matumizi yake muhimu ya kila siku na nauli ya kurudi nyumbani wakati wa likizo au dharura.

**VIFAA VYA KUTUMIA DARASANI NA WAKATI WA MITIHANI**

1. Ream ya Karatasi A4 mbili (**AINA YA DOUBLE "A" (Ni lazima kila mwaka).**
2. Mathematical set
3. Kamusi (English Dictionary)
4. Madaftari makubwa (Counter Books Quire four au three) yasiyopungua 10.

5. Scientific calculator ya " function kuanzia fx – 82MS to fx – 991MS (Kwa Kidato cha Tano michepuo ya **PCM, PGM, EGM,CBG,PCB na HGE). (Zinapatikana maeneo ya shule endapo utashindwa kupata huko uliko).**
6. Dissecting Kit" (Kwa wanafunzi wa Kidato cha Tano – Mchepuo wa **CBG (Zinapatikana maeneo ya shule endapo utashindwa kupata huko uliko).**

**ANGALIZO**: Mwanao aje na **Bima ya afya ya NHIF kama anayo** kwa wasio nayo Uongozi wa shule utaweka utaratibu wa matibabu Zingatia.

### C. Michango mbalimbali

**i. Malipo yafanyike kupitia Akaunti Na . 30301100043 – NMB**

**MUSOMA TECH .S.S**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 3 Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku na asubuhi ( Night & Monirning Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi **haruhusiwi kubadili dini** wala kumshawishi mwanafunzi **mwenzake kubadili dini** wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa tu**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. **Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule**;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xix. Kucheza michezo ya kihuni kama betting,Games(**Play station**) na mingine kama hiyo.

*Zingatia: mwanafunzi atakayepatikana na simu shuleni atafukuzwa shule mara moja na kulipa faini ya tsh.200, 000/=.*
*Pia shule yetu kwa sasa imefanyiwa ukarabati mkubwa na serikali.hivyo mwanafunzi akijihusisha na uharibifu wa mali ya umma ikiwemo kuchafua kuta kwa maandishi,kuvunja taa,vioo,milango n.k atalazimika kufidia gharama za uharibifu huo.*

KARIBU SANA MUSOMA UFUNDI

**MAWASILINO: 0755671818 MKUU WA SHULE / 0767 082905 (M/Mkuu wa Shule)**

**OFISI YA RAISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA**
**SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MUSOMA**

**FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI PAMOJA NA AHADI YA UTII WA SHERIA ZA SHULE**

1. Jina kamili ………………………………………………………

2. Anwani ya nyumbani ……………………………………………

3. Tarehe ya kuzaliwa ……………………………………….

4. Mahali ulipozaliwa,Kijiji/Mtaa………………..Kata……………..Tarafa…………….
   Wilaya………………………………….. Mkoa………………………………………

5. Mahali unapoishi kwa sasa Kijiji/Mtaa…………………….. Kata………………………Tarafa………………
   Wilaya………………………………….. Mkoa………………………………………

6. Shule ya Sekondari ulikotoka……………………………………….
   Anwani………………………………………………………………….

7. Dini/Dhehebu………………………………………………………..

8. Kabila………………………………………………………………….

9. Taifa (Mtanzania/Si Mtanzania………………………………………..

**10. JAMAA KATIKA FAMILIA AMBAO WANAWEZA KUPELEKEWA TAARIFA ZAKO MUHIMU KWA MASUALA YAHUSUYO SHULE:**

**(JAZA SEHEMU ZOTE NNE, PAMOJA NA PASSPORT SIZE ZA KILA MZAZI/MLEZI)**

Anaishi/ Haishi…………………………**Jina la Baba**………..Namba ya Simu…………

Kazi yake……………………………….Anwani……………………………

ii**) Jina la Mama**……………………………………Namba ya Simu ………

Anaishi/ Haishi…………………………………………………

Kazi yake…………………………………………… Anwani…………………………

iii) **Jina la Mlezi (1)**……………………………Uhusiano……………Namba ya Simu Kazi yake…………………………………………………

Anwani……………………………………………………………………………

iv) **Jina la Mlezi (2)**………………………. Uhusiano…………..
Namba ya Simu ………………… Kazi yake ………………………………
Anwani………………………………………

Mimi (Mwanafunzi)……………………………………………………..nathibitisha kuwa taarifa nilizozijaza hapo juu
ni za kweli. Ahadi yangu, Nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na shule hii na ninahaidi kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule.

……………………………………… …… …
Sahihi ya Mwanafunzi Tarehe

Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi)…………………………………………………………..
ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi ………………………………………………… nimeyasoma masharti na sheria za shule ya Sekondari Musoma ambako kijana wangu amechaguliwa kujiunga. Nahaidi kwamba nitamuhimiza mwanagu kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyoelezwa. Aidha nahaidi kushirikiana na uongozi katika malezi bora ya mwanagu ili baadae awe raia bora na mwema wa Taifa letu.

……………………. …………………..
Sahihi ya Mzazi/Mlezi Tarehe

**MUSOMA TECHNICAL SECONDARY SCHOOL**
**MEDICAL EXAMINATION FORM**
**MUSOMA TECHNICAL SECONDARY SCHOOL, P.O. BOX 54, MUSOMA.** Date…………………

To Medical Officer, …………………………………… …………………………………… ……
Ref……………………………………………………….. (NAME OF STUDENT)

Please examine the named Student as per Medical examination form below,

………………
**MAGITA G. NYANGORE**
**HEADMASTER**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

(To be completed by Government Medical Officer) Full
Name………………………………………………………………………………………..
Age……………….Height……………..(cm)Weight…………………………..(Kg)

1. Blood count (Red and White)…………………………………………
2. Stool Examination…………………………………………………………
3. Urinary analysis…………………………………………………………….
4. STDS and other V.D……………………………………………………
5. T.B and Leprosy test……………………………………………………
6. Eye test………………………………………………………………………
7. Ear test………………………………………………………………………
8. Chest …………………………………………………………………….
9. Abdominal test……………………………………………………………
10. Blood Group **(Very Crucial)**…………………………………………….
11. Spleen…………………………………………………………………………

Any additional defects or impairments, infections, chronic or family diseases (e.g Sickle cell),
…………………………………………………………………………………………………\
…………………………………………………………………………………………………\
…………………………………………………………………………………………………\
……………………………………………………………… I have examined the above named student and I certify that he/she is FIT/NOT FIT to pursue Secondary Education.
Signature…………………………………………Date…………………….
Station……………………………………………………………………
**Designation and Official Stamp………………………………………………**

**THANK YOU**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA**
**SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MUSOMA.**

**S.L.P 54 MUSOMA.**
**SIMU :0755671818, 0712658280.**
**E-mail :musomatechsecondaryschool@gmail.com**
**Web site: www.musomatech.sc.tz**

**YAH:MKATABA WA MAKUBALIANO KATI YA MWANAFUNZI NA SHULE KUHUSU KUFANYA VIZURI ZAIDI KITAALUMA**.

1. Mimi………………………………………..ninayesoma kidato cha……………..katika shule ya Sekondari ya Musoma Ufundi ninaahidi kusoma kwa bidii kwa lengo la kupata **Wastani wa A/B au Daraja la KWANZA/PILI** katika mitihani/majaribio na si vinginevyo. Hivyo ninasaini mkataba wa kupata **alama si chini ya 60** kwa kila somo ninalosoma Shuleni ili kuendana na **kauli mbiu ya Shule.** (PROSPERITY THROUGH TECHNOLOGY)

2. Ili kutimiza lengo hili: Nitahakikisha ninahudhuria vipindi vyote darasani,kufanya **mazoezi, majaribio,mitihani, na kazi mradi (Project Work)** bila kutegea na kwa wakati. Pia nitahudhuria **maandalizi ya masomo ya usiku** na **alfajiri** (**Night &Morning Preparation**) kama ambavyo uongozi wa Shule unavyoelekeza.

3. Nitakuwa tayari kuwajibishwa na uongozi wa Shule endapo nitaonyesha uzembe katika suala zima la taaluma shuleni ikiwa ni pamoja na kurudia mitihani/majaribio ambayo nitakuwa sikufikisha **Wastani wa alama 60** kwa gharama zangu mwenyewe na adhabu nyingine kadri mwalimu wa somo au Idara ya taaluma itavyoona inafaa kwa manufaa ya kunijenga kitaaluma.

4. Nitatii na kuheshimu ratiba za shule kwa ukamilifu na kwamba sitatoka nje ya shule bila ruhusa ya maandishi.

5. Nina apa kuwa Mimi sio mwizi na kwamba kamwe sita shiriki wala kuhisiwa kwenye tuko lolote la wizi

Mwisho, ninaahidi kutoa ushirikiano kwa Walimu wote na Wanafunzi wenzangu.

JINA LAMWANAFUNZI……………………………….TAHASUSI…………………

SAHIHI…………………… TAREHE…………………………………………………….

JINA LA MWANDAMIZI TAALUMA………………………………………………….

SAHIHI……………………TAREHE…………………………………………………….

**MKUU WA SHULE MUSOMA SEKONDARI** **KWA UFUATILIAJI**

**NAKALA:**
Mzazi

**VIFAA VYA USAFI ANAVYOPASWA KUNUNUA MWANAFUNZI KULINGANA NA TAHASUSI ALIYOCHAGULIWA.**

| Na. | TAHASUSI | JINA LA KIFAA. | IDADI |
|---|---|---|---|
| 1 | PCM | JEMBE LENYE MPINI | 01 |
| | | SOFT BROOM | 01 |
| | | | |
| 2 | PGM | PANGA | 01 |
| | | HARD BROOM | 01 |
| | | | |
| 3 | CBG | CHELEWA | 01 |
| | | Dawa ya choo Lita 5 | Lita 5 |
| | | | 01 |
| 4 | EGM | CHELEWA | 01 |
| | | SLASHER | 01 |
| | | | 01 |
| 5 | HGE | MIFAGIO YA BUIBUI | |
| | | HARD BROOM | 01 |
| | | | 01 |
| 6 | HGK | SLASHER | 01 |
| | | SQUIZER | 01 |
| | | | |
| 7 | HGL | NDOO YA KUDEKIA NA MOPA YAKE | 01 |

**Vifaa hvi vinapatikana karibu na Shule.**

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MUSOMA.**